**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA**

**MUHTASARI WA KIKAO CHA DHARURA CHA BODI YA ZABUNI KILICHO FANYIKA CHA TAREHE 04/10/2021 OFISI YA NSALALA- MBALIZI**

**MAHUDHURIO**

1. Ndg. Filbert mbwilo - Mwenyekiti
2. Ndg. Victor kilonzo - Katibu
3. Ndg. Beatrice Ngutu - Mjumbe
4. Ndg .Nicodemus Tindwa - Mjumbe
5. Ndg. Agnes elikunda - Mjumbe
6. Ndg. Aliko mbuba - Mjumbe

**SECRETARIETI**

1. Rebeca Msongole
2. Consesa Silayo

**AGENDA**

1. Kufungua kikao
2. kuidhinisha njia ya force account kutumika kwenye miradi ya ujenzi wa madarasa ya shule shikizi, ujenzi wa madarasa ya shule za sekondari, ujenzi wa wodi ya wagonjwa mahututi ICU hospitali ya wilaya inyala na ujenzi wa nyumba ya watumishi kituo cha afya Ikukwa.
3. Kufunga kikao

**Agenda Na.1: Kufungua Kikao**

Mwenyekiti alifungua kikao saa 4:10 asubuhi kwa kuwakaribisha wajumbe kwenye kikao.

**Agenda Na. 2: kuidhinisha njia ya force account kutumika kwenye miradi ya ujenzi wa madarasa ya shule shikizi ,ujenzi wa madarasa ya shule za sekondari , ujenzi wa wodi ya wagonjwa mahututi ICU hospitali ya wilaya inyala, na ujenzi wa nyumba ya watumishi kituo cha afya ikikwa.**

Halmashauri imepokea fedha kutoka serikali kuu kwa ajili ya miradi ya elimu na afya kama ifuatavyo:

i. Tsh 1,740,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya shule za sekondari
ii. Tsh 1,060,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya shule shikizi
iii. Tsh 250,000,000/= kwa ajilil ya ujenzi wa wodi ya wagonjwa mahututi ICU hospitali ya wilaya inyala
iv. Tsh 90,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya watumishi kituo cha afya Ikukwa

- **Sekretarieti** inaiomba bodi ya dhabuni iridhie miradi hii inayoendeshwa kwa njia ya force account.

**MAAMUZI YA BODI**

-Bodi ilipokea maombi ya sekretarieti na kuridhia miradi iendeshwe kwa njia ya force account.

**Agenda Na ,7:** Kufunga kikao

kikao kilifungwa saa 5:20 asubuhi.

..............................
Victor A. Kilonzo
Katibu

..............................
Filbert Mbwilo
Mwenyekiti

Tarehe 20/01/2022

## MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO KILICHOFANYIKA TAREHE 29.01.2022 KATIKA UKUMBI WA KIJIJI CHA INYALA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA

### MAHUDHURIO

**WAHESHIMIWA MADIWANI**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mh. Mwalingo M. Kisemba | - M/Kiti wa Halmashauri | -Mwenyekiti |
| 2. Mh. Ezekia S. Shitindi | - Makamu Mwenyekiti | -Mjumbe |
| 3. Mh. Flora L. Mwalwayo | - Diwani | -Mjumbe |
| 4. Mh. Julius C. Ntokani | - Diwani | -Mjumbe |
| 5. Mh. Andrew L. Mwaipopo | - Diwani | -Mjumbe |
| 6. Mh. Eng,Boniface S. Njombe | - Diwani | -Mjumbe |
| 7. Mh. Pili A. Mwantowe | - Diwani | -Mjumbe |
| 8. Mh. Oran M. Njeza | - Mbunge | -Mjumbe |
| 9. Mh. Maiko M. Mwanibhungu | - Diwani | -Mjumbe |
| 10.Ndg. Nicodemus Tindwa | - Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) | - Katibu |

**WATAALAM**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Ndg. Godfrey Chuwa | -K/Afisa Utumishi na Utawala (W) | -Mjumbe |
| 2. Ndg. Gerald E. Shayo | -Kaimu Afisa Nyuki (W) | -Mjumbe |
| 3. Ndg Agness F.Elikunda | -Afisa Maendeleo ya Jamii (W) | -Mjumbe |
| 4. Ndg. Rhoda Mahava | -Mweka Hazina (W) | -Mjumbe |
| 5. Ndg Musa Mwasile | -Kaimu Afisa Mipango (W) | -Mjumbe |
| 6. Ndg. Mary Makali | -Mthibiti Mkuu Ubora wa Shule (W) | -Mjumbe |
| 7. Ndg. Daudi Mwalusamba | -Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi (W) | -Mjumbe |
| 8. Ndg. Tanu Kameka | -Afisa Elimu Msingi (W) | -Mjumbe |
| 9. Ndg. Mdoe E. Mjema | -Kaimu Afisa Ardhi na Maliasili (W) | -Mjumbe |
| 10. Ndg. Beatrice Ngutu | -Afisa TEHAMA (W) | -Mjumbe |
| 11. Ndg .Dinday Njile | -Mkaguzi wa ndani (W) | -Mjumbe |
| 12. Ndg. Thereza Linda Deus | -K/Mwanasheria (W) | -Mjumbe |
| 13. Ndg. Dr Yahya Msuya | -Mganga Mkuu (W) | -Mjumbe |
| 14. Ndg. Jacques M. Kempanju | -K/A/Mazingira na U/Taka Ngumu (W) | -Mjumbe |
| 15. Ndg. Elizabeth Lyombe | -Afisa Biashara (W) | -Mjumbe |
| 16. Ndg. Langson Nsusa | -Kaimu Afisa Uchaguzi (W) | -Mjumbe |
| 17. Ndg. John T.Simwandiya | -Kaimu Afisa Elimu Sekondari (W) | -Mjumbe |
| 18. Ndg. Aidan Mlawa | -Kaimu Afisa Kilimo(W) | -Mjumbe |
| 19. Ndg. Aron M Sote | -Afisa Tarafa Isangati | -Mjumbe |
| 20. Ndg. Johnphace Makabe | -Karani wa Vikao | -K/Vikao |
| 21. Ndg. Stella John | -Karani wa Vikao | -K/Vikao |
| 22. Ndg. Faraja Osward | -Karani wa Vikao | -K/Vikao |



Scanned with CamScanner

## AGENDA

1. Kufungua kikao.
2. Kuthibitisha agenda.
3. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango wa tarehe 29.01 .2022.
4. Yatokanayo na Muhtasari wa kikao cha Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango wa tarehe 29.01 .2022.
5. Taarifa ya utekelezaji ya kamati ya Fedha Uongozi na Mipango kwa kipindi cha robo ya pili Mwezi Oktoba hadi Disemba 2021
   a) Taarifa ya utekelezaji wa kazi Idara ya Utumishi na Utawala kwa kipindi cha mwezi Oktoba2021,Disemba 2021
   b) Taarifa ya kitengo cha Uchaguzi
   c) Taarifa ya kitengo cha Sheria inayohusu usimamizi wa kesi mbalimbali
   d) Taarifa ya kitengo cha Tehama
   e) Taarifa ya kitengo cha Ugavi
   f) Taarifa ya Fedha na Biashara ya Mapato na Matumizi
   g) Taarifa ya Miradi ya Maendeleo
6. Taarifa ya Tathimini ya maombi ya mikopo ya wanawake na vijana na walemavu kwa robo ya tatu 2021/2022.
7. Taarifa ya Mradi wa urasimishaji wa makazi eneo la Mbalizi na Mwashiwawala kata ya Iwindi.
8. Taarifa ya Mkaguzi wa ndani kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba 2021 hadi Disemba 2021.
9. Taarifa ya ujenzi wa Nyumba ya Mkurugenzi na maombi ya fedha milioni 140 kwaajili ya ujenzi wa nyumba mbili za wakuu wa Idara.
10. Taarifa ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo
11. Mpango wa usimamizi uendeshaji wa shule ya sekondari ya wasichana Galijembe
12. Taarifa ya kukamilika kwa ujenzi wa vyumba 140 vya madarasa kwa fedha za uviko
13. mengineyo
14. Kukubaliana kuhusu maazimio ya kikao.
15. Kufunga kikao.

**KUMB.NA.MDC/FUM.40/2021/2022: KUFUNGUA KIKAO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ambaye aliwakaribisha wajumbe kwenye kikao, kisha alifungua kikao saa **11:08** asubuhi.

**KUMB.NA.MDC/FUM.41/2021/2022: KUTHIBITISHA AGENDA**

Wajumbe walithibitisha jumla ya agenda kumi na tano **(15)** ili ziweze kujadiliwa.

**KUMB.NA.MDC/FUM.42/2021/2022: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO WA TAREHE 10.12 .2021.**

Wajumbe walisoma muhtasari ukurasa hadi ukurasa hakukuwa na marekebisho. Kisha muhtasari ulithibitishwa na kusainiwa kuwa kumbukumbu sahihi za kikao.



Scanned with CamScanner

**KUMB.NA.MDC/FUM.44/2021/2022:YATOKANAYO NA MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO WA TAREHE 10.12.2022.**
Wajumbe walipokea yatokanayo na utekelezaji wake na kujadili kama ifuatavyo:-

Katika azimio **MDC/FUM.05/2021/2022** lililohusu Menejimenti iwasilishe mpango wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na timu za mapato zilizoundwa na kamati ya Fedha kwenye tarafa tatu. Wajumbe walipokea azimio na utekelezaji wake.

Katika azimio **MDC/FUM.06/2021/2022** lililohusu Menejimenti iwasilishe mikataba iliyoingiwa na Halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Halmashauri. Wajumbe walishauri baadhi ya marekebisho yafanyike kwenye mkataba kwa mfano mkataba umeandikwa wa mchanga ila ndani yake kuna kokoto hakuna viwango vya makubaliano ya malipo, umbali kutoka eneo la manunuzi mawe na mchanga havijaoneshwa vinahitajika kwa kiasi gani, mkataba haujaonesha unatoka kwa nani unaenda kwa nani, pia mkataba haujaonesha ni nani atakayekuwa msambazaji wa vifaa kisha kaimu mwanasheria alisema wameyachukua mapungufu yote kwa ajili ya utekelezaji.

**KUMB.NA.MDC/FUM.45/2021/2022:TAARIFA YA UTUMISHI NA UTAWALA MWEZI DISEMBA, 2021.**
Taarifa iliwasilishwa na Kaimu Afisa Utumishi na Utawala. Baada ya kuwasilishwa taarifa ilipitishwa.

**KUMB.NA.MDC/FUM.46/2021/2022:TAARIFA YA KITENGO CHA UCHAGUZI.**
Taarifa iliwasilishwa na kaimu Afisa Utumishi. Baada ya kuwasilisha mjumbe alitaka kujua kuhusu nafasi iliyoachwa wazi na Diwani aliyefariki. Katibu alisema taarifa imeshapelekwa Tume ya Uchaguzi na TAMISEMI wao ndio wanaotoa utaratibu wa kujaza nafasi wazi kisha taratibu zingine zinaendelea baada ya kuwasilishwa taarifa ilipitishwa.

**KUMB.NA.MDC/FUM.47/2021/2022; TAARIFA YA KITENGO CHA SHERIA.**
Taarifa iliwasilishwa na kaimu Mwanasheria alisema katika robo ya pili kesi zote bado zinaendelea hakuna kesi iliyofanyiwa maamuzi. Baada ya kuwasilishwa taarifa ilipitishwa.

**KUMB.NA.MDC/FUM.48/2021/2022;TAARIFA YA KITENGO CHA TEHAMA**
Taarifa iliwasilishwa na Afisa TEHAMA na baada ya kuwasilisha. wajumbe walishauri kama kuna watumishi wapo wenye Taaluma ya TEHAMA lakini wapo katika Idara nyingine wafanyiwe mabadiliko kazi/cheo ili kuondoa upungufu huo. Kisha taarifa ilipitishwa.

**KUMB.NA.MDC/FUM.49/2021/2022; TAARIFA YA KITENGO CHA UGAVI**
Taarifa iliwasilishwa na Kaimu Afisa Ugavi. Baada ya kuwasilishwa taarifa ilipitishwa.

**KUMB.NA.MDC/FUM.50/2021/2022: TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI.**
Taarifa iliwasilishwa na Kaimu Mweka Hazina kama ifuatavyo; sehemu ya kwanza ilikuwa ni mapato ya Halmashauri. Ambapo kwa mwaka wa fedha **2021/2022** ilikadiria kukusanya na kupokea jumla ya **Sh 60,734,020,306**. Kati ya fedha hizo **Sh 3,995,137,300** ni kutoka vyanzo vya ndani (Own Source) na **sh 56,738,637,006** ni ruzuku kutoka Serikali Kuu na wahisani.

Katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2021 Halmashauri imeweza kukusanya na kupokea **Sh 29,893,335,901** sawa na **49%** ya makadirio ambapo mapato toka vyanzo vya ndani ni **Sh 2,340,976,213** sawa na **59%** ya makadirio. Mapato fungwa ni sh **290,564,369** na ruzuku toka Serikali Kuu na Wahisani ni Sh **27,552,359,687** sawa na **49 %** ya Makadirio.



Scanned with CamScanner

Sehemu ya pili ni matumizi, ambapo kwa mwaka wa fedha **2021/2022**, Halmashauri ilipanga kutumia jumla ya **Sh. 60,734,020,306** ikiwa ni kwa ajili ya kugharamia shughuli za uendeshaji, mishahara ya watumishi na miradi ya maendeleo.

Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba Halmashauri imetumia **Sh 28,597,029,082** sawa na **47%** ya makadirio, ambapo matumizi ya mapato ya ndani ni **Sh 2,254,710,770.03** sawa na asilimia **56** ya makadirio. Matumizi mengineyo ni **Sh 549,633,033.44** sawa na asilimia 26 ya makadirio, matumizi kwa ajili ya mishahara ni **Sh 18,208,453,103.00** sawa na **26%** ya makadirio na matumizi ya miradi ya maendeleo ni **Sh 7,392,330,897.** sawa na **43%** ya makadirio. Baada ya kuwasilishwa taarifa ilipitishwa.

**KUMB.NA.MDC/FUM.51/2021/2022: TAARIFA YA MIRADI YA MAENDELEO.**

Taarifa iliwasilishwa na Kaimu Afisa Mipango na baada ya kuwasilisha mjumbe alishauri asilimia ya utekelezaji wa miradi iwe inaonyeshwa kwenye jedwali pia wajumbe walishauri taarifa ziboreshwe ili ziwe sahihi kwa sababu taarifa za mipango zinatumika katika idara mbalimbali za Halmashauri. Kisha taarifa ilipokelewa.

**KUMB.NA.MDC/FUM.52/2021/2022: TAARIFA YA TATHIMINI YA MAOMBI YA MIKOPO YA WANAWAKE NA VIJANA NA WALEMAVU ROBO YA PILI 2021,**

Taarifa iliwasilishwa na Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii. Baada ya kuwasilisha taarifa ilipitishwa.

**KUMB.NA.MDC/FUM/53/2021/2022; TAARIFA YA URASIMISHAJI WA MAKAZI ENEO LA MBALIZI NA MWASHIWAWALA KATA YA IWINDI.**

Taarifa iliwasilishwa na kaimu Afisa Nyuki baada ya kuwasilisha wajumbe walishauri kwenye sehemu ya wajibu ioneshe chuo kinawajibu wa kulipa Halmashauri. Pia kwenye mkataba ratiba ioneshe kuwa mkataba huo utachukua muda gani, mkataba uoneshe wajibu wa mkandarasi pia mjumbe alitaka kujua utaratibu wa malipo ukoje. Katibu alisema kwa kadiri viwanja vitakavyoendelea kurasimishwa hatutasubiri mwishoni ndipo Halmashauri ipate Fedha yake. Pia wajumbe walishauri miradi kama hii inapokuwa inatambulishwa viongozi wa kisiasa na wananchi wapewe taarifa ili nao waweze kushiriki sio mradi unafika mwisho na wao ndio wanajulishwa. Baada ya kuwasilishwa taarifa ilipitishwa.

**KUMB.NA.MDC/FUM/54/2021/2022;TAARIFA YA UKAGUZI WA NDANI**

Taarifa iliwasilishwa na Mkaguzi wa Ndani kuwa yale yaliyojadiliwa kwenye mkataba wa Halmashauri yafanyiwe kazi na stakabadhi ambazo bado hazijawasilishwa ofisi ya Mkaguzi ziwasilishwe ili aweze kuzihakiki baada ya kuwasilisha mjumbe alishauri menejimenti iwe inafuata taratibu za manunuzi ili kupunguza hoja. Baada ya kuwasilisha taarifa ilipitisha

**KUMB.NA.MDC/FUM/55/2021/2022; TAARIFA YA UJENZI WA NYUMBA YA MKURUGENZI NA MAOMBI YA FEDHA KIASI CHA SHILINGI MILIONI 140 KWAAJILI YA UJENZI WA NYUMBA MBILI ZA WAKUU WA IDARA**

Taarifa iliwasilishwa na kaimu Afisa Utumishi kwamba Halmashauri ilipokea fedha kiasi cha shilingi 150 kwa ajili ujenzi wa nyumba ya Mkurugenzi. Hivyo menejimenti inaomba kiasi cha shilingi 140 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba nyingine tatu za wakuu wa Idara. Baada ya kuwasilisha. Wajumbe walilidhia maombi haya kisha mjumbe alishauri menejimenti iharakishe mchakato wa ujenzi wa majengo hayo ili tuendelee kupokea Fedha zingine kuendelea na ujenzi wa nyumba nyingine za watumishi. Baada ya kuwasilishwa taarifa ilipitishwa.



Scanned with CamScanner

**KUMB.NA.MDC/FUM/56/2021/2022;TAARIFA YA UKAGUZI WA MIRADI.**

Taarifa iliwasilishwa na kaimu Afisa Mipango baada ya kuwasilisha, wajumbe walishauri maabara ya shule ya Sekondari Iwiji ikamilishwe kama walivyoelekeza wajumbe wa kamati ya fedha wakati wa ziara ili wanafunzi waanze kutumia maabara hiyo. Aidha kituo shikizi cha Ntinga madarasa yafanyiwe marekebisho na taarifa itolewe kikao kijacho. Mkaguzi wa ndani aende akafanye ukaguzi wa maabara shule ya Sekondari Iwiji, Mwakipesile, na shule ya Msingi Irambo pamoja na vituo shikizi vya Itete na Iwanza.

Mjumbe alishauri kwenye mradi wa Parachichi zichukukuliwe fedha za dharula ili eneo lizungushiwe uzio kuepuka miche ambayo imeshapandwa kuharibiwa na wanyama. Baada ya kuwasilisha taarifa ilipitishwa.

**KUMB.NA.MDC/FUM/57/2021/2022;MPANGO WA USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA GALIJEMBE**

Taarifa iliwasilishwa na Mwenyekiti wa Halmashauri. Baada ya kuwasilisha wajumbe waliijadili kwa kina kisha waliipitisha.

**KUMB.NA.MDC/FUM/58/2021/2022; TAARIFA YA KUKAMILIKA KWA UJENZI WA VYUMBA 140 VYA MADARASA KWA FEDHA ZA UVIKO 19**

Taarifa iliwasilishwa na kaimu Mhandisi wa Ujenzi. Baada ya kuwasilisha taarifa ilipitishwa.

**KUMB.NA.MDC/FUM.59/2021/2022: MENGINEYO**

Hapakuwa na mengineyo

**KUMB.NA.MDC/FUM.60/2021/2022: KUKUBALIANA KUHUSU MAAZIMIO YA KIKAO**

Wajumbe walikubaliana kuwa yafuatayo yawe maazimio ya kikao:-

1. Menejimenti ihakikishe inapeleka POS kwenye vijiji vyote ambayo vina makusanyo ya mkaa.
2. Menejimenti iwasilishe taarifa ya upimaji wa viwanja vya maeneo ya taasisi mbalimbali.
3. Menejimenti iweke kwenye Bajeti 2022/2023 miradi itakayoiingizia Halmashauri mapato na Mradi utakaowekezwa kwenye kiwanja cha Halmashauri kilichopo Block T.
4. Mkaguzi wa ndani aende akafanye ukaguzi wa maabara shule ya Sekondari Iwiji, Mwakipesile, na shule ya Msingi Irambo, vituo shikizi vya Itete na Iwanza.
5. Menejimenti ipitie miradi yote yenye mapungufu ya ukamilishaji ili ijulikane na Fedha zitengwe ili kukamilisha miradi hiyo.
6. Menejimenti iwasilishe mchakato wa kuanzishwa shule ya wavulana na wasichana katika Halmashauri kwa kutumia miundo mbinu ya Hosteli zilizopo kwenye shule za Iwiji, Izyira,Imezu,Isuto,Ilungu,Iwindi na Igoma.

**KUMB.NA.MDC/FUM.51/2021/2022: KUFUNGA KIKAO**

Kabla ya kufunga kikao Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michago yao katika kuhakikisha Halmashauri inasonga mbele. Baada ya hapo Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa 9:00 alasiri.

| | | |
|---|---|---|
| ..........[signature].......... | 28/02/2022 | ..........[signature].......... |
| KATIBU | TAREHE | MWENYEKITI |